

## Kuwa kama Mgomba wa Ndizi

Katika kazi ya Dignity, kila mara tunawaeleza watu kuwa kama miti. Tunachukua mfano kutoka kwa Isaya 61:3 katika Biblia ambapo Isaya anazungumzia watu kuwa kama miti mikuu ya haki. Basi iwapo watu ni kama miti, kuna swali rahisi la kujiuliza: Je, sisi ni miti ya aina gani? Mmishenari aliyefanya kazi kule Asia\* alisema kwamba watu ama kundi la watu ni kama Mgomba wa ndizi au Mbanyani.

Mti huu wa Banyan unapatikana barani Asia na unachukua eneo lote la mashambani au 'msitu'. Huota mizizi yenye nguvu na hivyo kutawala sehemu hiyo. Huchukua mwanga wote na maji na kwa sababu hiyo hakuna chochote ambacho kinaweza kumea chini yake. Mbanyani huchukua uhai wote.

Migomba ya ndizi ni tofauti sana. Inapokomaa, migomba hii inatengeneza miche ya "watoto" wa migomba, karibu nayo Mgomba mkubwa unasaidia "watoto" hadi pale itakapokua kibinafsi. Kisha mgomba uliokomaa hufa. Hupeana uhai wake ili mgomba mchanga ukue na kuzaa matunda yake.

Kwa kuzingatia hayo, Je wewe ni mti wa aina gani? Je wewe ni sehemu ya Kundi la Maisha au Kanisa la aina gani? Wakati mwingine Makundi ya Maisha huishia kuwepo kwa sababu za kibinafsi. Wanakutana, wanakuwa na wakati mzuri na kujifunza kwa pamoja. Hivi ni vitu vizuri vya kufanya lakini hatimaye wanalingana na aina gani ya mti? Je, wanajimarisha kama mbanyani au wanapeana uhai kwa wengine kama mgomba? Makundi mengine ya Uhai, yakiwepo na kujisadia yenyewe, pia huamua kuanzisha 'mtoto' wa makundi mpya sehemu mbalimbali. Wanachukua muda kuyakuza makundi haya hadi yawezekuimarika vya kutosha kukutana na kukua yenyewe. Wanatanguliza kuwasaidia wengine.


Wafilipi 2 inasema kwamba, "Yesu alikuwa na namna ya Mungu, ila hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu akatwaa namna ya mtumwa." Yesu kama mgomba wa ndizi hakushikilia maisha yake mwenyewe. Aliyapeana. Kwa kufanya hivyo aliumba maisha mapya kwingine. Alipeana uhai wake kwa ajili. Mgomba wa ndizi unatukumbusha haya. Mfano wa ajabu iliyoje na mfano wa kuigwa!

### Zingatia!

Katika Kikundi chenu cha Maisha, na kwa hakika Kundi lolote linao uwezo wa kuzalisha na kupanda kikundi kingine. Mnaweza kuanza kuomba na kutafuta namna ya kufanya hivyo pamoja. Fikirieni juu ya watu tofauti mnaowajua katika vijiji mbalimbali. Mnaweza kuchagua mtu mmoja au wawili kati yenu kupanga kundi jipya na kusaidiwa na wengine. Mnaweza kuamua kuwafunza watu ambao wanaweza kuanza makundi mengine. Kwa njia hii Kikundi chenu kitakuwa kama mgomba unaopeana uhai wake kwa ajili ya wengine.


### Omba:

- 1) Mungu atatusaidia kuishi kama mgomba wa ndizi!
- 2) Mnapowekeza maisha yenu kwa wengine, utatiwa moyo unapowaona wakikua.



Enock amejifunza jinsi ya kupanda Makundi ya Maisha. Alianzisha makundi mawili karibu na anakoishi. Makundi haya mawili yameweza kupanda Kikundi kimoja kila moja, sasa kuna makundi manne ya Maisha, hii inamaanisha takriban watu themanini wanaweza kujumuishwa katika jamii na kujifunza kuhusu Yesu kwa pamoja na kushiriki upendo wake na jamii pana.

**- Enock, Mwinilunga, Zambia**



Funzo hili limechochewa na: "Mgomba wa Ndizi" somo katika Panda.

Kwa maelezo zaidi:

[dignityonline.org.uk/publications](https://dignityonline.org.uk/publications)

\*HIEBERT, PG, Anthropological Reflections on Missiological Issues, Baker Books, 1994